

## **JAPAN IMEIPATIA TANZANIA MSAADA WA SHILINGI BILIONI 74.**

Serikali ya Japan imetoa msaada wa shilingi bilioni 74 kwa Serikali ya Tanzania, kwa ajili ya matengenezo ya upanuzi wa barabara ya Bagamoyo kuanzia eneo la Mwenge hadi Tegeta.

Makubaliano ya msaada huo yametiliwa saini baina ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi Bw. Ramadhan M. Khijjah na Balozi wa Japan nchini Tanzania Bw. Hiroshi Nakagawa.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa utiaji saini, Bw. Khijjah amesema “Japan wametupatia msaada huu mkubwa kusaidia utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa barabara ya Bagamoyo yenye urefu wa kilometa 12.9 kuanzia eneo la Mwenge hadi Tegeta”.

“Japan wametoa msaada huo mkubwa kwa wakati, kukamilika kwa barabara hiyo ambayo sasa itakuwa inapitisha magari mawili upande wa kulia na mawili upande wa kushoto kutasaidia kuondoa kero ya muda mrefu ya msongamano na foleni kubwa ya magari barabarani” alieleza Bw. Khijjah.

Aidha kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kuimarisha uchumi hasa katika nyanja ya biashara ambapo njia hiyo itatumika kuunganisha Dar es Salaam ambayo ni kitovu cha biashara na mikoa mingine tofauti na sasa ambapo barabara hiyo imekuwa kero kwa wananchi.

Naye Balozi wa Japan Bw. Hiroshi Nakagawa alisema upanuzi wa barabara hii hautaleti faida kwa wakazi wa Dar es Salaam tu bali na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Wakati huo Serikali imetia saini makubaliano na Serikali ya Japan ambapo Japan itaipatia Tanzania mkopo wa shilingi bilioni 108 kwa ajili ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 193 kati ya Tunduru - Namtumbo na Iringa hadi Dodoma.

**Imetolewa na Msemaji Mkuu  
Wizara ya Fedha na Uchumi  
31/05/2010**